HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MPANGO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA

MSITU WA MCHAKAMA

MPANGO HUU UMEANDALIWA NA SERIKALI YA KIJIJI CHA MCHAKAMA

AUGUST 2016

YALIYOMO

1: UTANGULIZI 3
1.1 Umiliki wa Msitu 3
1.2 Lengo Kuu la Mpango wa Usimamizi 3
1.3 Madhumuni 3
1.4 Mfumo wa Usimamizi 3
1.5 Muda wa Utekelezaji na Marekebisho ya Mpango 3
2: HISTORIA FUPI YA MPANGO KAZI 5
2.1 Jamii 5
2.1.1 Hali ya Kiuchumi na Kijamii 5
2.2 Maelezo kuhusu Msitu 5
2.2.1 Mahali ulipo Msitu na Ukubwa Wake 5
2.2.2 Vyanzo vya Maji 6
2.2.3 Hali ya Udongo 6
2.2.4 Uoto wa Asili na Mazingira. 6
2.2.5 Jamii za Miti ya Mbao 6
2.2.6 Mazao Yasiyotimbao 6
2.2.7 Wanyama Pori na Jamii za Mimea 7
2.3 Maeneo ya Usimamizi. 7
2.4 Matumizi ya Msitu 7
Mambo ya Asili & Haki za Kijadi 7
2.4.1 Historia ya Nyuma 7
2.4.2 Matumizi ya Sasa 7
3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU. 8
3.1 Matumizi ya Msingi 8
3.2 Matumizi Huru ya Msitu 8
3.3 Shughuli katika Misitu Zitakazotozwa Ushuru 8
3.4 Mazao Yanayohitaji Vibali vya Uvunaji 8
3.4.1 Utaratibu wa Kupata Leseni ya Uvunaji Miti ya Mbao. 9
3.4.2 Mazao Mengine ya Misitu Yatakayokatiwa Leseni 10
3.5 Matumizi Yasiyoruhusiwa ndani ya Msitu 10
4: HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU 11
4.1 Kijiji 11
4.1.1 Haki 11
4.1.2 Manufaa 11
4.1.3 Majukumu ya Serikali ya Kijiji 11
4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili 11
4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji 13
4.2 Halmashauri ya Wilaya 13
4.2.1 Haki 13
4.2.2 Manufaa 13
4.2.3 Majukumu 13

4.3 Serikali Kuu 14
4.3.1 Majukumu *14*
4.4 Mashirika yasiyo ya Kiserikali 14
4.41 Majukumu *14*
5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU 15
5.1 Mikakati ya Jumla ya Kuendeleza Msitu 15
5.2 Ulinzi wa Msitu 15
5.2.1 Ushirikishwaji wa Jamii katika Ulinzi wa Msitu *15*
5.2.2 Walinzi wa Doria *15*
5.3 Kusafisha Mpaka na Barabara za Moto 15
5.4 Kurudisha hali ya Msitu 16
5.4.1 Kutokana na Machipukizi (Uoto wa asili) *16*
5.4.2 Upandaji wa miti kwenye maeneo yaliyo wazi *16*
5.4.3 Palizi kwenye maeneo yaliyopandwa miti *16*
6: MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU 17
6.1 Vyanzo vya Mapato 17
6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau 17
6.3 Matumizi ya Mapato 17
6.4 Ukusanyaji na Utunzaji wa Fedha 17
6.4.1 Vitabu Muhimu vya Kutunza Kumbukumbu Vinavyotakiwa *18*
6.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi *18*
6.4.3 Kuwajibishwa *18*
7: UFUATILIAJI NA TATHIMINI 19
7.1 Ufuatiliaji 19
7.2 Tathimini ya Kati na ya Mwisho 19
KIAMBATISHO A : RAMANI ZA KIJIJI NA MSITU 20
Ramani inayoonyesha Mipaka ya Kijiji *20*
Ramani inayoonyesha Mipaka ya Msitu wa Kijiji *21*
KIAMBATISHO B : MPANGO WA UTEKELEZAJI 22
Kazi za Kila Mwaka *23*
Kazi za Mwaka wa Kwanza *23*
Kazi za Mwaka wa Pili *23*
SHERIA NDOGO 24

SURA YA KWANZA

1: UTANGULIZI

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 inatoa kipaumbele kwa jamii kushirikishwa katika usimamizi wa misitu. Pia sera inasisitiza mchango wa sekta ya misitu katika kukuza kipato cha jamii ili kupunguza umasikini. Mwaka 2002 serikali ya Tanzania ilipitisha sheria mpya ya misitu ambayo inaipa mamlaka jamii zinazoishi kandokando ya misitu kusimamia misitu yao. Mchakama kimeandaa mwongozo wa matumizi endelevu wa Msitu wa Kijiji. Matumizi haya yameainishwa katika mpango kazi huu.

Mpango huu ni mwongozo wa shughuli zote zitakazofanyika katika kipindi cha kutumika kwa mpango na shughuli hizo zimefafanuliwa na kuwekwa bayana. Shughuli hizo ni uboreshaji wa msitu, kuanzisha utaratibu wa usimamizi, udhibiti wa uvunaji haramu, usimamizi wa sheria za misitu na ukusanyaji na usimamizi wa mapato na matumizi yatokanayo na rasilimali za msitu. Kutakuwa na utunzaji wa kumbukumbu za shughuli zote zilizofanyika ili kuendana na matakwa ya mpango. Kumbukumbu zote zitapatikana pia katika Halmashauri ya Wilaya. matukio mbalimbali yatokanayo na msitu. Sheria ndogo zitatungwa ili kusimamia utekelezaji wa mpango.

Mpango huu umeandaliwa na kamati ya maliasili ya kijiji cha Mchakama, timu ya wawezeshaji kutoka Halmashauri ya Wilaya Kilwa chini ya Mpango wa Taifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kwa kushirikiana na Shirika la Kuhifadhi Mpingo na maendeleo. Mpango huu utatumika katika kipindi cha miaka mitano cha umiliki wa msitu.

1.1 Umiliki wa Msitu

Kijiji cha Mchakama kinamiliki msitu wa Uchungwa Msitu wa Kijiji cha Mchakama ulitengwa kuwa hifadhi 2012 chini ya usaidizi wa kitalaamu toka kwa wawezeshaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na wawezeshaji wa Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo.

1.2 Lengo Kuu la Mpango wa Usimamizi

Msitu wa Uchungwa una lengo la kulinda, kuhifadhi, na kufanya uvunaji endelevu kwa kuvuna mazao ya mbao, mazao timbao na rasilimali zingine za misitu kiendelevu. Lengo kuu likiwa ni kuweka msitu katika hali ya uasilia na kuboresha hali ya maisha ya kizazi kilichopo na kijacho.

1.3 Madhumuni

Kuboresha hali ya maisha ya wanajamii wa kijiji cha Mchakama kwa;

- Kuhifadhi eneo lenye ukubwa wa hekta 5,639 la Msitu wa Kijiji cha Mchakama dhidi ya ukataji miti ovyo, uharibifu na matumizi yasiyofaa.
- Kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji wa mazao yasiyo timbao kwa wakati wote kwa ajili ya matumizi ya kawaida.
- Kijiji cha Mchakama kupata mapato kutokana na biashara ya rasilimali za misitu ili kuboresha maisha ya wanakijiji wake.

1.4 Mfumo wa Usimamizi

Usimamizi misitu ya asili unaofuata uvunaji endelevu na upandaji wa miti ya asili na utunzaji wa machipukizi na udhibiti wa moto kwa kufuata mpango uliopo.

1.5 Muda wa Utekelezaji na Marekebisho ya Mpango

i. Huu ni mpango wa miaka mitano. Mpango huu utarekebishwa na Kamati ya Maliasili mwishoni mwa mwaka wa pili au muda wowote endapo kuna umuhimu

wa kufanya hivyo. Hakutafanyika mabadiliko yeyote katika mpango huu bila ya kibali cha Halmashauri ya Wilaya.

ii. Baada ya kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji, mpango huu utafanyiwa maboresho/marekebisho

iii. Mapendekezo ya Maboresho yataandaliwa na kujadiliwa na kamati ya Maliasili, na kuwasilishwa kwenye Halmashauri ya kijiji, na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

iv. Kamati ya maliasili na Halmashauri ya kijiji wanapaswa kushauriana na Afisa Misitu wilaya, na/au wadau wengine wa maswala ya misitu, kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya Mpango wa Usimamizi wa Misitu wa kijiji kwa ajili ya kupitishwa na mkutano mkuu.

v. Afisa Mtendji wa kijiji akishirikiana na kamati ya maliasili, ataandaa taarifa za mabadiliko ya Mpango wa Usimamizi wa Misitu, na kuziaambatanisha na muhtasari wa Mkutano mkuu wa kijiji uliothibitisha mabadiko hayo, na kuziwasilisha katika Ofisi ya misitu wa Wilaya.

SURA YA PILI

2: HISTORIA FUPI YA MPANGO KAZI

2.1 Jamii

Mchakama kipo katika kata ya Mandawa, tarafa ya Pande katika Wilaya ya Kilwa. Kina idadi ya watu wapatao1788 katika kaya zipatazo 406 (sensa ya mwaka 2012). Kila kaya ina wastani wa watu kati ya 4 na kina kilomita za mraba zipatazo 13,655.91. Kilisajiliwa mwaka 1976 kabla kitongoji cha mavuji.

Kijiji cha Mchakama kinapakana na kijiji cha Mavuji kilichopo kata ya Mandawa katika upande wa mashariki, kwa upande wa magharibi kinapakana na kijiji cha Liwiti kilichopo kata ya Likawage, kwa upande wa Kaskazini kinapakana na Kijiji cha Migeregere na Kusini kinapakana na kijiji cha Kiwawa kilichopo kata ya Mandawa. Pia kijiji kimepakana na msitu wa hifadhi wa serikali Mitundumbea kwa upande wa magharibi kusini.

Kijiji hakina Cheti cha Ardhi ya Kijiji lakini mipaka inajulikana vizuri na Kijiji kina muhtasari wa makubaliano kuhusu mipaka pamoja na vijiji vyote vinavyopakana na Mchakama. Mipaka ya kijiji imewekwa mawe ya kuonyesha alama za mipaka. Angalia Kiambatisho A. Ramani ya inayoonyesha ardhi ya Kijiji katika Wilaya ya Kilwa.

Vitongoji vya Kijiji vinavyotambulika ni: Mchakama na Mkundi, kati ya vitongoji hivyo kitongoji cha mchakama kipo karibu na msitu wa hifadhi wa kijiji.

2.1.1 Hali ya Kiuchumi na Kijamii

Wanajamii walio wengi ni wakulima. Wengine hujishughulisha na ufugaji wa n'gombe, mbuzi, kondoo, kuku, na biashara ndogo ndogo kama vioski, magenge namigahawa.

Mazao makuu yanayozalishwa Kijijini kwa ajili ya chakula ni Mpunga, Mahindi, Mtama, Mihogo, Kunde na choroko.

Mazao makuu yanayozalishwa kijijini kwa ajili ya biashara ni Ufuta, Korosho, nyanya, vitunguu, kabechi, Karanga, pilipili hoho na matikiti.

Mapato yatokanayo na kilimo kwa kila kaya ni kati ya Tsh 250,000/= na Tsh 400,000/= kwa mwaka.

Wakulima hujipatia pato la ziada kutokana na urinaji wa asali, uvunaji mbao, uuzaji wa mbogamboga, ufugaji kuku, mbuzi na utegaji wanyama.

Kila kaya ina wastani wa watu 4-7.

Huduma za jamii zinazopatikana Kijijini ni Msikiti, kanisa, Kituo cha afya na ofisi ya kijiji.

Wananchi huteka maji toka kwenye mto mavuji ambapo kwa miguu ni mwendo wa dakika *2* toka katikati ya Kijiji.

Mji ulio jirani na Kijiji ni Kivinje ambao unafikika kwa usafiri wa gari, pikipiki, baiskeli, kwa mwendo wa saa moja na dakika tano mpaka masaa 2.

2.2 Maelezo kuhusu Msitu

Jina la msitu ni *Uchungwa*

2.2.1 Mahali ulipo Msitu na Ukubwa Wake

Msitu wa Kijiji cha Mchakama una ukubwa wa hekari 5639 na upo upande wa Kaskazini katika ardhi ya kijiji. Unapakana na Kitongoji cha Mchakama. Kitongoji kilicho karibu zaidi na Msitu

ni Mchakama. Kiambatisho A, mchoro unaoonyesha alama za mipaka ya msitu na mahali ulipo katika ramani ya kijiji.

Msitu unafikika kwa gari kupitia barabara ya Mchakama, Mavuji, mpaka Naulai. Kwa miguu ni Nandembo, Mitomani, Chila, Kilombani, Ndyanje hadi Uchungwa

Matumizi ya maeneo yanayozunguka msitu ni kama ifuatavyo;

- Upande wa kaskazini matumizi hayajulikani kwa jamii kwani msitu upo mbali na upande wamashariki matumizi ni upasuaji mbao.
- Upande wa kusini matumizi ni utegaji wa wanyama pori na upasuaji mbao na magharibi matumizi nako hayafahamiki.

2.2.2 Vyanzo vya Maji

Msitu huu ni chanzo cha maji na hutiririsha maji yake katika;

- Mto Mavuji ambao maji yake hutumika katika maeneo ya Mchakama na Mavuji

Kuna mito ifuatayo katika msitu huu;

- Mito mitatu (Machemba, Manganje na Mpamande) ambayo maji yake hutumika katika maeneo ya Mchakama na Mavuji.

(Uvunaji hauruhusiwi katika eneo la mita 30 toka kingo za mito.)

Pia kuna vijito/mito midogo vifuatavyo katika msitu huu

- Vijito vitatu (Noro, Nakaato na Laini) ambayo maji yake hutumika katika maeneo ya Noro, Mchakama na Namatimbili

(Uvunaji hauruhusiwi pia katika eneo la mita 20 toka kingo za mito midogo inayotiririsha maji kwa mwaka mzima)

2.2.3 Hali ya Udongo

Aina ya udongo katika msitu huu ni Kichanga.

Hali ya tabaka la udongo (geology)

Hali ya kijiografia ya msitu ni ni milima, tambarare na mabonde.

2.2.4 Uoto wa Asili na Mazingira.

Sehemu kubwa ya msitu ni tambarare.

Uoto wa asili ni wa miombo (misitu ya mataji wazi). Miti mifupi ya miombo ndio inayopatikana kwa wingi zaidi na kuna vichaka vya miiba na uwanda wa misitu ya pwani.

2.2.5 Jamii za Miti ya Mbao

Kuna aina nyingi za jamii tofauti za miti katika msitu wa Kijiji. Jamii za miti ya thamani ya mbao zilizopo msituni ni Mpingo (*Dalbergia melanoxylon*), Mtondoro (*Julbernardia globiflora*), Mlondondo (*Xeoderis stuhlmannii*), Mninga jangwa(*Pterocarpus angolensis*), Mnangu, Mnepa(*Pteleopsis myrtifolia*), Mseni, Mkongo(*Afzelia quanzensis*), Mpangapanga(*Millettia stuhlmannii*), Msufi pori(*Bombax rhodognaphalon)*, Mlipa deni(*Sterculia conloba*), Miombo*(Brachystegia longifolia),* Mnidu(*Cordyala africa*na), Msekeseke(*Bobgunnia madagascariensis*)

2.2.6 Mazao Yasiyotimbao

Kuna aina mbalimbali za mazao yasiyo timbao kama vile asali ya nyuki, uyoga, matunda pori, wanyama pori, madawa ya asili na kamba.

Miti inayofaa kwa ujenzi ni Mtandawala na Msenjele, Miti ya matunda ni Mgongo, Mtopetope, Mfuru, misofu na vitoe. Miti inayotumika kutengenezea kamba ni Mchenga na Myombo.

Jamii za uyoga zifuatazo zinapatikana katika msitu huu Uyoga-ndembo, Nguyugu, Upoa, Mbuyu, Ngolowele, Mlelema na Mchinji.

2.2.7 Wanyama Pori na Jamii za Mimea

Wanyama wanaopatikana katika msitu huu ni pamoja na tembo, nyati, nyani, mbwa mwitu,nguruwe, chui na simba. Vilevile wanapatikana nyoka wakali kama Ranga (nyoka jangwa), Boma, Kobra, Chatu mlima na Mtunguru (kijani njano).

2.3 Maeneo ya Usimamizi.

Msitu huu umegawanyika katika maeneo madogo ya usimamizi, kuna eneo lenye ukubwa wa hekari 629 ambalo ni asilimia 10 ya msitu mzima na limetengwa kama eneo ambalo uvunaji wa mazao ya misitu hauruhusiwi kabisa kufanyika katika eneo hili kwani eneo hili ni muhimu kwa mimea adimu hasa mmea ya Mnungunungu na pia eneo hili lina asili ya misitu ya ukanda wa pwani (Misitu iliyofunga na isiyopukutisha majani kwa kipindi cha mwaka mzima na kuwa haiungui moto kwa sababu hakuna nyasi nyingi).

Eneo la pili ni eneo ambalo halipo katika asilimia kumi lakini lina asili ya msitu wa ukanda wa pwani (Misitu iliyofunga na isiyopukutisha majani kwa kipindi cha mwaka mzima na kuwa haiungui moto kwa sababu hakuna nyasi nyingi) eneo hili litaruhisiwa kuvumwa lakini kwa utaratibu wa kutambua maeneo yaliyofanyiwa uvunaji kwa kuchukua alama za GPS na eneo lenye miti zaidi ya mitatu yenye sifa za uvunaji mti mmoja utavunwa. Maeneo haya yameonyeshwa katika kiambatanisho A kwenye ramani ya msitu wa Kijiji.

2.4 Matumizi ya Msitu

Msitu utachangia katika kuinua uchumi kwa kuuza rasilimali za mazao ya msitu. Msitu utatumika katika Uhifadhi na matumizi endelevu ya mazao ya msitu. Msitu utachangia katika kutoa huduma za msingi za jamii kama vile ujenzi wa nyumba; Shule, Zahanati, Msikiti na Kanisa.

2.4.1 Mambo ya Asili & Haki za Kijadi

Hakuna matumizi yoyote ya kijadi ambayo hufanyika ndani ya msitu.

2.4.2 Historia ya Nyuma

Awali msitu ulikuwa unatumika kwa ajili ya kupata asali na kuwinda wanyama. Historia inaonyesha hakukuwa na shughuli za kilimo na uvunaji mbao.

2.4.3 Matumizi ya Sasa

Msitu huu kwa sasa ni Msitu wa Hifadhi wa Kijiji ambapo Kamati ya Maliasili ndio meneja wa usimamizi wa Msitu. Matumizi ya sasa yatakayofanyika katika Msitu wa kijiji cha Mchakama ni; uvnaji endelevu, uhifadhi wa vyanzo vya maji na bionuwai na matumizi ya mazao ya timbao yanayofuata utaratibu ulio pangwa na kijiji pamoja na uokotaji wa kuni.

SURA YA TATU

3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU.

Msitu utasimamiwa kama msitu wa asili na kutakuwa na mabadiliko kiasi katika usimamizi huo ili kuepuka kubadilisha hali ya uasilia wa msitu. Taratibu za kuingia msituni na za matumizi ya mazao ya msitu yameelezewa katika sheria ndogo za usimamizi wa msitu wa kijiji cha Mchakama . Wale ambao hawatafuata taratibu hizi watapigwa faini kulingana na na sheria ndogo za usimamizi wa misitu za kijiji cha Mchakama.

3.1 Matumizi ya Msingi

Wanajamii wa kijiji cha Mchakama watakuwa na haki ya kuingia katika Msitu wa Kijiji bila kibali na kupita njia zinazofahamika, haki hii itahusu vijiji jirani vya Liwiti,Nainokwe,Mavuji na Migeregere. Wanajamii pia watakuwa na haki ya kuchota maji katika msitu.

Wasio wakazi wa kijiji hawataruhusiwa katika maeneo ya kijadi bila uangalizi wa kamati ya Maliasili.

3.2 Matumizi Huru ya Msitu

Matumizi huru kwa wanakijiji wa Mchakama yatakuwa kwa ajili ya mazao yasiyotimbao kama vile uyoga, matundapori, mbogamwitu, kuni, nyasi na madawa ya asili, vyote hivyo vitapatiwa kibali maalum cha bure toka mjumbe wa kamati ya maliasili kwa kushirikiana na mwenyekiti wa kitongoji. Wasio wakazi wa kijiji cha Mchakama wanaweza pia kuomba kibali toka kamati ya maliasili ya kijiji kutumia mazao yaliyotajwa hapo juu. Kamati ya maliasili itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mazao haya yanatumiwa kiendelevu. Watumiaji wa nje ya kijiji wanaotaka kuvuna mazao haya kwa ajili ya biashara wanaweza kutozwa ushuru kama ilivyopangwa na Kamati ya Maliasili.

Kibali cha kutundika mizinga ya nyuki kitatolewa bure kwa kijiji cha Mchakama

Wanajamii toka vijiji vya Liwiti,Nainokwe,Migeregere na Mavuji wanaruhusiwa kuendelea kufanya shughuli zao za kimila(matambiko na miti ya mila) bila pingamizi lolote.

3.3 Shughuli katika Misitu Zitakazotozwa Ushuru

Kutakuwa na ushuru wa serikali ya Kijiji kwa shughuli zifuatazo msituni;

- Kutembelea msitu kwa ajili ya mafunzo
- Utafiti
- Utalii msituni

Viwango vya ushuru vimeonyeshwa katika Kiambatisho C. Watalaam na wawezeshaji ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia kufanikisha kwa mpango huu hawatahusika na kutozwa ushuru.

3.4 Mazao Yanayohitaji Vibali vya Uvunaji

Kabla ya kuvuna jamii yeyote ya miti iliyoorodheshwa, lazima tathmini ifanyike ili kubaini kiasi kilichopo na mpango wa uvunaji utatayarishwa. Tathmini ya kina itafanyika kufuatana na mwongozo wa Tathmini Shirikishi ya rasilimali za misiti wa Idara ya Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Taarifa za Tathmini shirikishi zimeambatanishwa katika mpango huu. Tathmini shirikishi haitafanyika katika eneo lililotengwa kwa ajili ya hifadhi (eneo la 10% la msitu).

Mpango wa uvunaji utaelezea namna kiwango cha uvunaji kilivyopatikana kutokana na matokeo ya tathmini na utabainisha ni kwa namna gani kiwango hicho ni endelevu. Mpango wa uvunaji ni lazima upitishwe na kamati ya maliasili na kuambatanishwa katika mpango huu.

Taarifa ya tathmini shirikishi ya Msitu wa Uchngwa

Kiasi cha Kuvuna Kiendelevu katika Msitu	**KKT**	**KMK**	**Ujazo (m^3)**	**Ujazo(m^3) kwa Mwaka**
Mseni	484	19	1118	223.6
Mnangu	623	0	1450	290
Mlondondo	286	0	377	75.4
Mtondoro	63	11	266	53.2
Mpingo	27	11	29	5.8
Mpangapanga	207	0	420	84
Msufi pori	241	0	729	145.8
Mkongo	145	0	360	72
Msekeseke	51	0	73	14.6
Mnepa	299	0	593	118.6
Mnidu	58	0	162	32.4
Miombo	48	0	70	14

Hakuna jamii yeyote ya miti itavunwa pasipo uendelevu, mbali na jamii za miti zilizoorodheshwa katika kipengele 2.2.5 juu hakuna jamii yeyote ya miti itavunwa kwa biashara katika kipindi chote cha utekelezaji wa mpango. Kama Kijiji cha Mchakama kitahitaji kuruhusu uvunaji wa jamii ambazo hazikuorodheshwa katika mpango huu, itabidi kijiji kiandike barua ya maombi ya kuvuna kwa Afisa Misitu wa Wilaya. Kabla ya kuidhinisha uvunaji Afisa Misitu wa Wilaya ya Mchakama atajiridhisha kama Tathimini ya kina na mpango wa uvunaji kwa ajili ya jamii hizo imefanyika. Kama tathmini haijafanyika Afisa Misitu kwa kusaidiana na kijiji watafanya tathimini na kuandaa mpango wa uvunaji. Baada ya kupata kibali cha maandishi toka kwa Afisa Misitu wa Wilaya uvunaji utafanyika..

3.4.1 Utaratibu wa Kupata Leseni ya Uvunaji Miti ya Mbao.

Utaratibu huu utahusisha miti yote iliyoorodheshwa katika kipengele 2.2.5 juu au iliyofanyiwa tathimini na kuandaliwa mpango wa uvunaji endelevu.

1 Uvunaji utafanyika kwa kufuata Mwongozo wa uvunaji katika misitu ya vijiji wa mwaka 2013 uliotolewa na Wizara ya Malaisili na Utalii.Mtu yeyote anayetaka kuvuna mazao ya misitu toka Msitu wa Kijiji lazima kwanza aandike barua ya maombi kijijini na aonyeshe aina na kiasi anachotarajia kuvuna. Pia atajaza fomu ya Maombi ya uvunaji na lazima awe amekidhi mashariti ya Kuwa mfanyabiashara wa mazao ya Misitu kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za uvunaji.

- Kamati ya Maliasili itajadili na kupitisha ombi hilo endapo itaridhia kufuatana na matakwa ya mpango wa usimamizi na mpango wa uvunaji. Kama mpango wa uvunaji haujaandaliwa kibali hakitatolewa na uvunaji hauruhusiwi.
- Kama bei haijaainishwa katika mpango wa uvunaji, Kamati ya Maliasili itapanga bei ya kuvuna mazao ya misitu na bei hizo kupitishwa na Serikali ya Kijiji lakini bei itakayopangwa isiwe chini ya kiwango kilichowekwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002 .

- Kamati ya Maliasili wakishirikiana na Serikali ya Kijiji pamoja na Afisa Misitu wa Wilaya watapanga bei ya mabaki yaliyoachwa Msituni baada ya uvunaji.
- Mwombaji atalipa gharama za leseni kwa Kamati ya Maliasili na kupatiwa stakabadhi halali ya malipo.
- Mwombaji atawasilisha stakabadhi ya malipo kwa Afisa Misitu wa Wilaya ambaye atampatia leseni ya kuingia msituni na kuvuna zao lililokubaliwa.
- Wanakijiji wa Kijiji Mchakama watakaohitaji mbao kwa ajili ya ujenzi watalipia asilimia 20 ya bei iliyoelekezwa na Serikali kwa kila mita moja ya ujazo na itafanyiwa marekebisho wakati wa mapitio ya mpango wa usimamizi wa Msitu. Fursa hii ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba Kijijini Mchakama Kamati ya maliasili itasimamia na kukadiria kiasi cha mbao kitakachohitajika kwa ajili ya ujenzi na kukakgua nyaraka za kiwanja pamoja na ujenzi kwa wale watakaotuma maombi ya kujenga nyumba ya mteja.
- Mwombaji atarudi tena kijijini na kuwasilisha leseni kijijini, Kamati ya Maliasili itamwonyesha eneo la kuvuna mazao ya misitu anayoyahitaji.
- Baada ya kuvuna magogo yote yaliyokatwa na visiki yatagongwa nyundo ya kijiji.
- Mwisho mwombaji lazima apate kibali cha kusafirishia toka kwa Afisa Misitu wa Wilaya ili aweze kusafirsha mazao yake bila usumbufu nje ya Wilaya. Kibali hiki hutolewa bure na lazima kiwasilishwe kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji ambaye ataweka kumbukumbu ya nambari ya kibali kabla mzigo haujatolewa kijijini.
- Utaratibu huu utafuatwa kwa ununuzi wa mabaki ya magogo, vilingu na mazao mengine ya misitu yatakayovunwa kibiashara.

3.4.2 Mazao Mengine ya Misitu Yatakayokatiwa Leseni

- Kijiji hakitaruhusiwa kutoa leseni au vibali vya uwindaji wa Wanyamapori, vibali na leseni vitatolewa na Afisa Wanyamapori wa Wilaya au serikali Kuu.

3.5 Matumizi Yasiyoruhusiwa ndani ya Msitu

- Kilimo ndani ya msitu.
- Kukata kuni mbichi
- Uchakataji wa mbao na magogo kwa kutumia chainsaw;
- Uvunaji katika eneo la asilimia 10 ya Msitu(eneo lisilo la uvuna) au katika maeneo ya chanzo cha maji - mita sitini kutoka kingo za mto kama ilivyoainishwa katika kipengele 2.2.2 hapo juu;
- Malisho ya mifugo ndani ya msitu.
- Makazi ndani ya msitu.
- Uvunaji wa miti ya mbao ambayo haijaorodheshwa katika kipengele 2.2.5 juu au miti ambayo haijatengenezewa mpango wa uvunaji.
- Uvunaji katika eneo la hifadhi au katika maeneo muhimu ya kimila na jadi.
- Kuchoma moto ovyo.
- Uanzishwaji wa njia mpya zisizo rasimi ndani ya msitu.
- Uzalishaji mkaa.
- Uchimbaji mdogo wa madini.
- Uwindaji wa wanyama ambao wako hatarini kutoweka

SURA YA NNE

4: HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU

Msitu wa kijiji cha Mchakama una wadau wafuatao; Serikali ya Kijiji, Halimashauri ya Wilaya ya Kilwa, serikali kuu na wadau wengine. Majukumu ya kila mdau yameelezewa kama ifuatavyo:

4.1 Kijiji

4.1.1 Haki

- Kumiliki na kutunza msitu wa Kijiji.
- Kukamata, kupiga faini au kumshitaki mtu yeyote anayeenda kinyume na sheria ndogo za kijiji zilizopitishwa na mpango huu.
- Kutumia rasilimali kama ilivyobainishwa katika mpango wa Usimamizi wa Misitu.
- Kukusanya na kutumia ushuru na mapato mengine yatokanayo na mazao ya misitu katika shughuli za maendeleo ya jamii na hivyo kuboresha hali za maisha ya wanajamii.
- Kufanya maamuzi juu ya usimamizi na matumizi ya msitu.

4.1.2 Manufaa

- Kutumia mazao ya misitu bila mashariti magumu kama ilivyoainishwa katika mpango wa usimamizi shirikishi misitu.
- Kutumia miti na mbao kwa ajili ya ujenzi na ukarabaji wa huduma za jamii kijijini.
- Mapato yatokanayo na faini na ushuru wa mazao ya misitu ni mali ya kijiji ingawa kunaweza kuwa na makubaliano ambapo Halmashauri ya Wilaya itapata gawio fulani kutokana na huduma za uwezeshaji kama ilivyobainishwa katika kipengele 7.2.
- Kupata mafunzo ya kitaalam katika masuala mbalimbali ya usimamizi misitu na kuboresha maisha ya jamii.

4.1.3 Majukumu ya Serikali ya Kijiji

- Msimamizi mkuu wa shughuli zote za utunzaji wa msitu.
- Kuthibiti mapato na matumizi yote yatokanayo na msitu.
- Kutatua migogoro inayohusiana na misitu pale inapojitokeza na kupeleka matatizo hayo ngazi ya Halmashauri ya Wilaya pale yanaposhindikana kutatua kijijini.
- Kutunga, Kuboresha na Kusimamia utekelezajki wa sheria ndogo na Mpango wa Usimamizi wa Msitu wa Kijiji ..
- Kuhakiki vibali vyote vilivyotolewa na Kamati ya Maliasili.
- Kupokea taarifa za uharibifu wa msitu toka Kamati ya Maliasili na wanakijiji kwa ujumla na kuzifanyia kazi.
- Kujadili na kupitisha mipangokazi ya mwaka ya Msitu wa Kijiji iliyoandaliwa na kamati ya Maliasili.
- Kujadili na kuidhinisha mapendekezo ya matumizi yote ya fedha kwa kamati ya Maliasili, doria,na wajumbe wa serikali ya kijiji kwa ajili ya shughuli za msitu.

4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili

Kamati ya Maliasili ina majukumu yafuatayo:

- Kuratibu shughuli zote za msitu kama vile; upandaji miti, ukusanyaji wa mazao ya misitu na kutunza kumbukumbu za msitu.
- Kutoa vibali vya uvunaji wa mazao ya misitu.
- Kuhakikisha doria imefanyika kila mara na kwa uhakika.
- Kuandaa mpango wa kazi wa mwaka wa shughuli za msitu.
- Kutathmini rasilimali za misitu na kutengeneza mpango wa uvunaji.
- Kutoa taarifa za maendeleo na uharibifu wa msitu kwa serikali ya kijiji.
- Kusimamia na kufuatilia uvunaji.
- Kuratibu shughuli zote zinazofanyika msituni.
- Kupendekeza na kusimamia sheria ndogo ikiwemo kuzirekebisha inapohitajika.
- Kuijulisha jamii juu ya matukio katika Msitu wa Kijiji na maeneo yanayozunguka.
- Kuielimisha jamii juu ya mabadiliko ya miongozo mbalimbali ya utunzaji misitu.
- Kutoa taarifa ya robo, nusu na mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa misitu kwa Afisa Misitu wa Wilaya.
- Kutoa taarifa ya robo mwaka kwa Halmashauri ili kuendana na utaratibu mpya wa kuweka kumbukumbu.

4.1.4.1 Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili

- Kusimamia shughuli zote za Kamati ya Maliasili ikiwa ni pamoja na vikao
- Kuitisha mikutano ya Kamati
- Kuwa msemaji mkuu wa Kamati
- Kusaini Mihtasari yote ya vikao vya Kamati
- Kuhakikisha kuwa Katibu anaweka kumbukumbu sahihi kuhusu vibali, mipango kazi, taarifa za mrejesho, mapato, doria na faini
- Kuhakikisha kuwa taarifa zinaifikia Serikali ya Kijiji

4.1.4.2 Katibu wa Kamati ya Maliasili

- Kuweka kumbukumbu za Kamati
- Kuandaa agenda za mikutano
- Kuandika mihtasari ya vikao vinavyofanywa na Kamati
- Kutoa taarifa za Kamati kwenye Serikali ya Kijiji
- Kutoa vibali vya uvunaji baada ya kupitishwa na Serikali ya Kijiji
- Kuratibu shughuli za doria
- Kuwaalika wajumbe kwenye mikutano baada ya kuwasiliana na Mwenyekiti wa Kamati
- Kutekeleza shughuli nyingine zozote atakazo agizwa na Kamati kupitia Mwenyekiti.
- Kusoma taarifa za mapato na matumizi ya Kamati.

4.1.4.3 Muweka Hazina wa Kamati ya Maliasili

- kutunza vitabu vya kumbukumbu vya fedha za Kamati

- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi kwa Kamati ya Mailiasili kila mwezi
- Kupokea mapato yanayotokana na mazao ya msitu na kutoa stakabadhi
- Kusaini stakabadhi na risiti zote zinazohusiana na malipo ya fedha.

4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji

- Kuzuia uharibifu wowote utakaojitokeza katika msitu kama vile uchomaji moto na uvunaji holela wa mazao ya misitu.
- Kutoa taarifa ya uharibifu wa aina yeyote utakaofanyika ndani ya msitu kwa Kamati ya Maliasili na serikali ya Kijiji.
- Kushiriki katika shughuli zote za kuboresha msitu.
- Kupitia na kuidhinisha inapofaa sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili.
- Kushiriki katika kulinda msitu na kutoa msaada kwa timu ya doria mara kwa mara.
- Kupokea au kudai na kujadili taarifa zinazohusu maendeleleo ya Msitu, mapato na matumizi na baadae kupitisha au kutoa maelekezo kwa Halmashauri ya Kijiji au Kamati ya Maliasili
- Kupitia, kuboresha na kuidhinisha mpango wa usimamizi wa Msitu na sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili na Halmashauri ya Kijiji

4.2 Halmashauri ya Wilaya

4.2.1 Haki

- Kupokea taarifa za mwezi, robo na nusu mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa msitu.
- Kukagua vitabu vya mapato na matumizi na kuchukua hatua zinazotakiwa kama italazimu.
- Kurudisha mamlaka ya usimamizi wa msitu chini ya halmashauri ya wilaya kama kijiji kitashindwa kuusimamia ipasavyo.

4.2.2 Manufaa

- Kupungua kwa gharama za usimamizi wa misitu.
- Kuboreka kwa usimamizi wa misitu.
- Kupungua kwa migogoro na migongano inayohusiana na matumizi ya misitu kati ya Halmashauri ya Wilaya na jamii.
- Kuboreka kwa usimamizi wa misitu na hivyo kudhibiti ufyekaji wa Misitu na kupunguza uharibifu wa Misitu;

4.2.3 Majukumu

- Kupitisha Mpango wa Usimamizi Misitu, Sheria ndogo na Mpango wa uvunaji.
- Kuhalalisha mazao yatokanayo na Msitu wa Kijiji.
- Kutoa watalaam kwa ajili ya shughuli za msitu pale inapohitajika.
- Kusaidia kutafuta soko la mazao ya Misitu.
- Kusimamia na kutatua migogoro ambayo iko juu ya uwezo wa Serikali ya Kijiji.

- Kuongoza zoezi la kubaini fursa na vikwazo katika kipindi cha kwanza na cha mwisho cha mpango huu.
- Kuingilia kati kama kuna jambo au shughuli yeyote imefanyika kinyume cha utaratibu wa mpango kazi.
- Kufuatilia na kushauri au kuchukua hatua wakati wote wa utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa Msitu na mpango wa uvunaji wa Msitu;
- Kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na Misitu yanatumika vizuri na Kijiji kama ilivyopitishwa na Mkutano mkuu wa Kijiji.

4.3 Serikali Kuu

4.3.1 Majukumu

- Kutoa watalaam washauri pale wanapohitajika.
- Kutunga Sheria, Sera na kutoa miongozo mbalimbali inayohusu usimamizi misitu.

4.4 Mashirika yasiyo ya Kiserikali

4.41 Majukumu

- Kutafuta masoko ya mazao ya Msitu
- Kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa Msitu
- Kutoa msaada wa kitaalamu na kusaidia uendeshaji wa shughuli za kuendesha Msitu
- Kuwezesha kufanya tathimini za rasilimali za Misitu pale itakapohitajika
- Kufuatilia na kutoa ushauri wa utekelezaji wa shughuli za kuendeleza Msitu

SURA YA TANO

5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU

Mambo yatakayoangaliwa ni pamoja na upandaji wa miti na utunzaji wa machipukizi dhidi ya moto, ulinzi wa msitu, kinga na uthibiti wa moto pamoja na mipango ya muda mrefu ya matumizi endelevu wa mazao ya msitu. Mwongozo wa mpango wa utekelezaji wa miaka mitano umeonyeshwa katika kiambatisho B.

5.1 Mikakati ya Jumla ya Kuendeleza Msitu

Katika kuendeleza msitu, mikakati ifuatayo imewekwa;

- Kuthibiti uchomaji moto ovyo msituni.
- Kuthibiti malisho ya mifugo msituni
- Kufanya doria za mara kwa mara ili kuthibiti uvunaji holela na uharibifu mwingine wa msitu.
- Kusafisha mipaka ya msitu.

5.2 Ulinzi wa Msitu

Usimamizi wa Msitu wa Kijiji utakuwa chini ya serikali ya kijiji na utatunzwa na wanajamii.

5.2.1 Ushirikishwaji wa Jamii katika Ulinzi wa Msitu

Msitu utalindwa na wanajamii wote wanaozunguka wanaopakana na mstitu. Kila mtu atatoa taarifa kwa uongozi wa kijiji au kamati ya maliasili au kikosi cha doria pale anapoona uharibifu katika msitu. Kamati ya maliasili itaratibu na kusimamia shughuli za doria.

5.2.2 Walinzi wa Doria

Kutakuwa na timu ya doria itakayochaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji ambayo itakuwa na jukumu la kufanya doria za mara kwa mara katika msitu wa jamii. Kikosi cha doria kitakachokuwa kama ifuatavyo:-

- Kamanda mmoja wa kikosi
- Wajumbe wawili wa Kamati ya Maliasili.
- Wanajamii watatu wenye uelewa wa masuala ya misitu

Doria inaweza kuwa ya wanakikosi wawili hadi sita, na kila doria lazima awepo mjumbe mmoja wa kamati ya maliasili, na mwanajamii mmoja. Kikosi cha doria kitaweka kumbukumbu zote za doria katika kitabu cha doria na kitatoa taarifa za matukio kwa kamati ya maliasili baada ya doria. Doria itafanyika angalau mara moja kwa wiki. Wanadoria watalipwa posho kutokana na makubaliano yatakayofanyika.

Kikosi cha doria kitachaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji. Kamanda wa kikosi cha doria atakuwa na sifa zifuatazo; mtu shupavu ambaye ni mwaminifu. Wanakikosi watabadilishwa na mkutano mkuu wa kijiji kila baada ya miezi sita au wakati wowote inapobidi kufanya hivyo.

Wanakikosi cha doria watakaobainika kutokuwa waaminifu watafukuzwa mara moja na wengine watachaguliwa kujaza nafasi zao.

5.3 Kusafisha Mpaka na Barabara za Moto

Kamati ya maliasili ya kijiji na jamii kwa ujumla watashiriki katika kusafisha mpaka wa msitu na kutengeneza barabara za moto. Kamati ya maliasili itaamua wapi barabara za moto zipite baada ya kupata ushauri toka kwa Afisa Misitu wa Wilaya. Ubabuaji moto ni hatua mojawapo muhimu katika kuthibiti moto, na hili ni jukumu la kamati ya maliasili na wanajamii kwa

ujumla. Zoezi la ubabuaji na usafishaji wa barabara za moto ni kazi ngumu inayohitaji fedha toka vyanzo mbalimbali.

5.4 Kurudisha hali ya Msitu

5.4.1 Kutokana na Machipukizi (Uoto wa asili)

Njia hii hutegemea miche iliyoota yenyewe kutokana na mbegu, mashina au mizizi ya miti iliyovunwa.

5.4.2 Upandaji wa miti kwenye maeneo yaliyo wazi

Maeneo yote yaliyo wazi ndani ya msitu ambayo yanaonekana ni vigumu uoto wa asili kujaza yatapandwa miti inayokubaliana na mazingira hayo hasa ile iliyokuwepo lakini ikaadimika kutokana na matukio ya moto ya mara kwa mara na uvunaji holela uliokuwa ukifanyika kipindi cha nyuma.

5.4.3 Palizi kwenye maeneo yaliyopandwa miti

Palizi ya kisahani itafanyika mara moja kwa mwaka ili kuhakisha miche iliyopandwa haisongwi na majani au mimea mingine.

SURA YA SITA

6: MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU

6.1 Vyanzo vya Mapato

Kutakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo toka msitu wa jamii:

- Ushuru
- Ada za leseni
- Ada za vikundi vilivyoko mafunzoni, shughuli za utafiti na utalii
- Faini za wahalifu
- Na Mengineyo

6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na mazao ya msitu utakuwa kati ya serikali ya kijiji na Halmashauri ya Wilaya. Mgawanyo huu utazingatia nani mwenye majukumu makubwa zaidi katika kutunza na kuendeleza msitu. Halmashauri ya wilaya watapewa asilimia 5%MCDI na 5% Halmashauri ya Wilaya ya mapato ya msitu , kamati ya maliasili asilimia 40 na Serikali ya kijiji asilimia 50. Kila mwaka Serikali ya kijiji itatoa kiasi fulani cha mapato yatokanayo na rasilimali za misitu kwa Halmashauri ya Wilaya kulingana na huduma ambazo Halmashauri imetoa.

6.3 Matumizi ya Mapato

Mapato yatokanayo na msitu yataelekezwa katika shughuli za;

- Kuendeleza shughuli za msitu zilizopangwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Mapato yatakayobaki yatapelekwa kwa serikali ya kijiji ili yatumike katika shughuli za jamii.

Matumizi halali ya mapato yatokanayo na msitu wa jamii ni:

- Kulipa motisha (posho) kwa doria.
- Kununua vifaa muhimu kwa ajili ya kuendeleza shughuli za msitu kama ilivyobainishwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Matumizi mengine ya ziada ya kuendeleza msitu yaliyoidhinishwa na Serikali ya Kijiji.
- Ununuzi wa vitabu kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za shughuli za msitu.
- Kuchangia katika shughuli za maendeleo kijijini.
- Asilimia 40 ya mapato yatakuwa kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa msitu chini ya Kamati ya Maliasili ya Kijiji.

6.4 Ukusanyaji na Utunzaji wa Fedha

Fedha zote zitatunzwa benki isipokuwa kwa fedha chache kwa ajili ya matumizi madogodogo. Pesa ndogondogo haitakiwi kuzidi shilingi 50,000/=. Kutakuwa na akaunti benki itakayofunguliwa kwa jina la Kamati ya Maliasili Mchakama. Kutakuwa na watia sahihi wanne; Afisa Mtendaji wa Kijiji (A), Mjumbe mmoja wa Kamati ya Mipango ya Kijiji (A), Mwenyekiti (B) na mweka Hazina wa Kamati ya Maliasili ya kijiji (B). Mtia sahihi mmoja wa A na mmoja wa B watahitajika kuchukua pesa toka benki.

6.4.1 Vitabu Muhimu vya Kutunza Kumbukumbu Vinavyotakiwa

Mweka Hazina wa Kamati ya Maliasili atakuwa na jukumu la kutunza vitabu vya kumbukumbu. Vitabu vinatakiwa kuwa tayari kwa ukaguzi wakati wowote na vitakaguliwa na;

- Kamati ya fedha na mipango ya serikali ya kijiji.
- Mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya Wilaya.

Vitabu vitakavyokaguliwa ni;

- Jalada la kumbukumbu/muhitasari wa vikao.
- Kitabu cha kumbukumbu za doria kinachoonyesha tarehe ya doria, njia iliyotumika, kama kuna wahalifu waliokamatwa na dalili zozote za kuwepo kwa uharibifu wa msitu.
- Kitabu cha kumbukumbu za uhalifu kinachoonyesha majina ya wahalifu, faini zilizolipwa, tarehe na nambari ya stakabadhi.
- Vitabu vya vibali na leseni vinavyoonyesha nambari ya kibali, mpewaji, sababu ya kibali, kiasi cha mzigo, kiasi cha fedha, nambari ya stakabadhi, tarehe na jina la mwanakamati aliyesimamia.
- Kitabu cha stakabadhi za malipo yote yaliyofanyika kulingana na mpango kazi huu.
- Kitabu cha matumizi madogo madogo kwa ajili ya kumbukumbu za matumizi ya pesa ambazo hazikuwekwa katika akaunti ya benki.

6.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi

Kamati ya Maliasili itatoa taarifa ya Mapato na Matumizi kila mwezi kwa Serikali ya Kijiji. Pia kila baada ya miezi mitatu Serikali ya Kijiji itatoa taarifa za Kamati ya Maliasili katika mkutano mkuu wa kijiji ambapo Kamati ya Maliasili nayo inaweza kuwakilisha taarifa.

6.4.3 Kuwajibishwa

Mwanakamati au mwanakijiji yeyote atakayepatikana na kosa la kutumia vibaya fedha za msitu atawajibishwa na serikali ya kijiji au atashitakiwa katika Baraza la usuluishi la kata au Mahakama ya mwanzo. Mjumbe yeyote wa Kamati ya Maliasili atakayepatikana na kosa lazima ajiuzulu haraka na uchaguzi mpya utafanyika kumchagua mjumbe mwingine kuziba pengo hilo.

SURA YA SABA

7: UFUATILIAJI NA TATHIMINI

7.1 Ufuatiliaji

Serikali ya Kijiji itafuatilia shughuli zote zilizopangwa kulingana na mpango kazi wa kila mwaka katika kipindi chote cha miaka mitano. Ufuatiliaji huu utahakikisha kuwa shughuli zote zimefanyika kulingana na mpango kazi.

7.2 Tathimini ya Kati na ya Mwisho

Zoezi la kubaini fursa na vikwazo litafanyika ili kuelewa hali ya maendeleo kama ilivyobainishwa katika mpango kazi huu. Zoezi hili litafanyika mwishoni mwa mwaka wa pili, na mwishoni mwa kipindi cha miaka mitano.

Tathimini itafanyika kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la utekelezaji wa mpango kazi lililoonyeshwa katika kiambatisho B. Zoezi hili la tathmini litaongozwa na Afisa Misitu wa Wilaya chini ya mpango wa kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A : RAMANI ZA KIJIJI NA MSITU

Ramani inayoonyesha Mipaka ya Kijiji



Ramani hapo juu inayoonyesha mipaka ya Kijiji cha Mchakama Vijiji vinavyopakana na Mchakama vimeonyeshwa, mawe ya mipaka yameonyeshwa kwa alama ya pembetatu na kupewa nambari. Vipimo vya GPS (UTM37L : WGS84) katika mawe ya mipaka ni kama ifuatavyo;

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
1.		8996629	517018
2.		9001921	520520
3.		8997013	533174
4.	...	8991235	534503
5.	...	8990724	530848
6.		8991670	529646
7.		8992335	529467
8.		8993025	528700
9.		8992744	527320
10.		8992692	526885

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
11.		8987145	523639
12.		8984844	519497
13.		8986123	520162
14.		8989753	520776
15.		8992820	519523

Ramani inayoonyesha Mipaka ya Msitu wa Kijiji



Ramani hapo juu inayoonyesha mipaka ya Msitu wa Kijiji cha Mchakama, maeneo yenye Misitu ya ukanda wa pwani na eneo la asilimia kumi. Eneo la asilimia kumi ni eneo la uhifadhi ambapo uvunaji hauruhusiwi kabisa. Vipimo vya GPS (UTM37L: WGS84) katika mawe ya mipaka ni kama ifuatavyo;

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
1.	...	516984	8996513
2.	...	520521	9001801
3.	...	526068	8999653
4.	...	526643	8998679
5.	...	526282	8997179
6.	...	526016	8996287
7.	...	525358	8995882
8.	...	525029	8994588
9.	...	525321	8993895
10.	...	524801	8993358
11.	...	524732	8993763
12.	...	523789	8993321
13.	...	523400	8992528
14.	...	523228	8993118
15.	...	522783	8992761
16.	...	522204	8993086
17.	...	521802	8993729
18.	...	520981	8993423
19.	...	520633	8993948
20.	...	520163	8994320
21.		518911	8993291

KIAMBATISHO B : MPANGO WA UTEKELEZAJI

Kila mwaka kamati ya maliasili ya kijiji ni lazima iandae mpango kazi kwa mwaka unaofuata.

Kazi za Kila Mwaka

- Doria za mara kwa mara
- Kubabua moto
- Kusimamia matumizi ya sheria ndogo (Serikali ya Kijiji)
- Kuweka kinga za moto (Kamati ya Maliasili)
- Kuweka barabara za moto (Wanajamii/Kamati ya Maliasili)
- Ulinzi wa Msitu (jamii nzima)
- Kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya misitu (Kamati ya maliasili)

Kazi za Mwaka wa Kwanza

- Kubabua moto au kusafisha mipaka kuzunguka msitu (Jamii na Kamati ya maliasili)
- Kujenga kituo cha ukaguzi wa mazao ya misitu (Kamati ya maliasili)
- Doria za mara kwa mara
- Kusimamia matumizi ya sheria ndogo (Serikali ya Kijiji)
- Kuweka kinga za moto (Kamati ya maliasili)
- Ulinzi wa Msitu (jamii nzima)
- Kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya misitu (Kamati ya maliasili)
- Kuweka mabango ya kupiga vita vitendo haramu na kuonyesha msitu.

Kazi za Mwaka wa Pili

- Doria za mara kwa mara
- Kubabua
- Kusimamia matumizi ya sheria ndogo (Serikali ya Kijiji)
- Kuweka kinga za moto (Kamati ya maliasili)
- Kuweka barabara za moto (Wanajamii/Kamati ya Maliasili)
- Ulinzi wa Msitu (jamii nzima)
- Kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya misitu (Kamati ya maliasili)

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA MAMLAKA ZA WILAYA

(SURA 287)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 168

SHERIA NDOGO ZA KUTUNZA, KUSIMAMIA RASILIMALI ZA MSITU WA KIJIJI CHA MCHAKAMA

Jina la Sheria	1	Sheria hizi zitaitwa sheria ndogo za kutunza, kusimamia na kutumia Rasilimali za msitu wa kijiji cha Mchakama
Tarehe ya kuanza kutumika	2	Sheria hizi zitaanza kutumika mara baada kupitishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Kilwa
Tafsiri	3	**"Msitu wa kijiji**"maana yake ni eneo la msitu lililotengwa na Kijiji lenye miti na uoto mwingine wa asili linalomilikiwa na Kijiji cha Mchakama.

"Mpango wa Usimamizi wa Misitu" maana yake ni kabrasha lenye maelezo ya namna jamii ya kijiji cha Mchakama kitakavyo kuwa kina tunza,simamia na kutumia rasilimali za msitu.

"Halmashauri ya kijiji" maana yake ni zaidi ya wajumbe 15 wa serikali ya kijiji cha Mchakama

"Mkutano mkuu wa kijiji" maana yake ni mkutano wa Wananchi wote wa Kijiji cha Mchakama wenye Mamlaka na maamuzi ya mwisho katika kijiji cha Mchakama. Ni kikao cha kijiji kinachohudhuriwa na Wanakijiji wote wenye akili timamu na wenye umri usiopungua miaka 18.

"**Kamati ya Maliasili ya Kijiji"** Maana yake ni kamati iliyochaguliwa na kuundwa na serikali ya kijiji kupitia mkutano mkuu wa Kijiji cha Mchakama ambayo majukumu yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu misitu iliyopo ndani ya mipaka ya kijiji na maliasili nyingine zilizomo kwenye kijiji cha Mchakama

"Meneja wa msitu" maana yake ni kamati ya maliasili ambayo kazi yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu Msitu.

"**Mwanakijiji"** Maana yake ni mtu yeyote aliyeandikishwa kwenye orodha ya wakazi wa Kijiji na pia anatmbulika na serikali ya Kijiji cha Mchakama kuwa mwanakijiji wa kijiji cha Mchakama

"Kijiji" maana yake ni Kijiji cha Mchakama pamoja na Vitongoji vyake.

"Kiongozi" Mtu yeyote aliyepewa madaraka na mamlaka na wananchi ili awatumikie

4

UTARATIBU WA JUMLA WA KUTUMIA MSITU NA MAZAO YA MISITU

I. Watu ambao wanaruhusiwa kuingia katika msitu wa kijiji kwa shughuli mbalimbali za usimamizi kutokana na taratibu zilizokubalika ni wakazi wa Kijiji cha Mcakama tu.

II. Watu wengine kutoka nje ya kijiji cha Mchakama wataruhusiwa Kuingia ndani ya Msitu wa Kijiji kwa vibali maalum na endapo watakuwa na shughuli iliyokubalika.

III. Kwa wale wanakijiji wasiojiweza ambao wanatambuliwa na Serikali ya Kijiji kama vile wagonjwa wa kudumu, Walemavu na Wazee watachukua mazao ya msitu yasiyo ya biashara bure bila kutozwa ushuru wa aina yeyote.

IV. Mahitaji madogomadogo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kama vile uyoga matundapori, mbogamboga, kuni, na ukindu hapatakuwa na malipo ila kutakuwa na siku Maalum itakayo pangwa na mkutano mkuu wa kijiji ya kukusanya mazao hayo, siku hiyo inaweza kubadilika kutokana na matakwa ya jamii.

Sheria ya Misitu 2002 na Sura ya 283

5 Mazao yote ambayo ni kwa ajili ya biashara yatavunwa kwa kulipia ushuru na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Sheria ya Misitu **na** Sheria ya Wanyama Pori.

6 Vibali vitatolewa na kamati ya Maliasili ya Kijiji, katibu wa kamati ndio atakua mwandishi wa vibali, ikiwa hayupo mtu yeyote ndani ya kamati atakayependekezwa na kamati atafaa kuandika vibali hivyo .Vibali vyote vitakuwa vinagongwa Muhuri maalumu uliothibitishwa na Serikali ya Kijiji.

7 (i) **Matumizi ya fuatayo yataruhusiwa bila kibali wala ushuru/ada**

a) Njia za miguu zinazopita msituni
b) Kuokota kuni kavu kwa ajili ya matumizi ya nyumbani
c) Uyoga, matunda, mbogapori na madawa ya asili, kukata minyaa na nyasi za kuezekea kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.
d) Kukata nyasiza kuezekea kwa matumizi ya nyumbani.
e) Matambiko pamoja na shughuli za kimila na jadi.

(ii) Matumizi yaliyoruhusiwa kwa kibali maalum

a) Kutundika mizinga na uvunaji wa asali
b) Kutumia mazao ya misitu kwa ajili ya maendeleo ya huduma za jamii kama vile ukarabati/ujenzi wa shule, zahanati n.k
c) Kuchimba dawa za asili chini ya usimamizi wa kamati ya maliasili

(iii) Matumizi yaliyoruhusiwa kwa kulipiwa ushuru/ada

a) Kuvuna miti kwa ajili ya majengo
b) Kuwinda wanyamapori
c) Kuwinda ndege
d) Kuvuna magogo
e) Kuingia ndani ya msitu kwa ajili ya kufanya utafiti wa mafunzo au utalii.

Bila kuathiri kifungu kidogo cha (b) (c) utaratibu wa kuwinda wanyama pori na kuvuna magogo ni ule uliowekwa na Sheria ya Wanyama pori na Sheria ya Misitu.

(iv) Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu

a) Kuchoma moto ovyo msitu
b) Kukata na kupasua miti ya mbao iliyozuiliwa
c) Kutega wanyamapori ambao si waharibifu wa mazao ya Kilimo.
d) Kuharibu uoto wa asili sehemu yeyote katika msitu
e) Kuvuna asali kwa kutumia moto.
f) Shughuli za kilimo
g) Makazi ya watu
h) Kuchoma mkaa.
i) Utupaji wa taka ngumu na kemikali ndani ya msitu wa hifadhi
j) Kuchunga mifugo,ngombe na mbuzi

k) Kuchimba madini,mawe,kokoto na mafuta.
l) Kuanzisha njia za miguu au gari zisizo rasmi.

(v) Viwango vya ushuru

(i) Kufanya mafunzo au utafiti ndani ya msitu shilingi zisizopungua 20,000/kwa mgeni na Mtanzania 10,000/- kwa siku ushuru huo utalipwa kwa kundi zima. Watakaowaongoza watalipwa 7,000/- kila mmoja.

(ii) Kufanya utalii ndani ya msitu ni shilingi zisizopungua 50,000/- Kila mtalii mmoja ambaye ni mgeni ,kwa Mtanzania atalipa 25,000/[-kwa siku.Waongozaji watalipwa Shs. 7,000/- kila Mmoja kwa siku moja.

8

VIWANGO VYA ADHABU NA FAINI

a) Mtu yeyote atakaye patikana analima, anatega wanyama, anaweka makazi au anachoma misitu atalipa faini isipungua Shilingi 50,000/- na isiyozidi shilingi 300,000/- au kifungo kisicho zidi miezi sita au vyote faini na adhabu
b) Mtu yeyote akipatikana na magogo, mbao au nguzo bila ya kibali atalipa faini isiyopungua shilingi 50,000/- na isiyozidi shilingi 300,000/- au kutumikia kifungo kisichozidi miezi sita au vyote faini na adhabu.Atakayekamatwa kwa kosa la kukata mianzi au fito atalipa faini isiyopungua shilingi 10,000/-.Nguzo shilingi 30,000/-

c) Mtu yeyote akipatikana anawinda wanyama au kuchoma mkaa ndani ya msitu bila ya kibali faini isiyopungua shilingi 50,000/- na isiyozidi shilingi 300,000/- au kutumikia kifungo kisicho pungua miezi sita au vyote faini na adhabu.

d) Mtu yeyote akipatikana anaondoa au kubadili alama za msitu zilizo wekwa atakuwa ametenda kosa na atalipa faini isiyopungua shilingi 50,000/- na isiyozidi shilingi 300,000/- au kutumikia kifungo kisicho pungua miezi sita au vyote faini na adhabu

e) Mtu yeyote akipatikana anachimba mawe au madini ndani ya msitu bila ya kibali atalipa faini isiyopungua shilingi 50,000/- na isiyozidi shilingi 300,000/- au kifungo kisicho pungua miezi sita au vyote kwa pamoja kifungo na faini.

f) Mtu yeyote akipatikana anarina asali sehemu yeyote ndani ya eneo la msitu bila kibali atalipa faini isiyopunga shilingi 50,000/- na isiyozidi shilingi 300,000/- au kifungo kisicho pungua miezi sita au vyote kifungo na faini.

g) Mtu yeyote akipatikana anaingia msituni bila kibali maalum kwa shughuli zakukata kuni mbichi, kuchuna magome ya miti, kufanya biashara, kuchukua dawa za tiba, matunda, miyaa, ukindu, uyoga,fito, kongowele. udongo, nyasi, miswaki, pikicho au mboga atalipa faini kwa kila kosa kiasi kisichopungua shilingi 35,000/-. au kifungo kisicho pungua miezi mitatu au kifungo na faini vyote kwa pamoja.

h) Kuchunga mifugo ndani ya msitu bila ya kibali faini kwa kila mnyama kiasi kisichopungua shilingi 10,000/-kwa kila kichwa cha ngombe na shilingi 5,000/-kwa kila kichwa cha mbuzi au kondoo.

i) "kiongozi" akipatikana na hatia ya kuhusika katika kukiuka mojawapo ya taratibu zilizowekwa na sheria hii fani yake ni kiasi kisichopungua shilingi 50,000/-pamoja na kufukukuzwa toka kwenye uongozi au kupelekwa mahakamani kulingana na kosa.

j) Mtu yeyote ambaye atakataa kulipa faini au kujaza fomu atapelekwa mahakamani kwa hatua zaidi.

k) Vitu vyote vitakavyokamatwa ikiwa ni pamoja na mbao,magogo,wanyama, kutokana na makosa yaliyotajwa katika vifungu (a-l) vitataifishwa na kuuzwa kwa njia ya mnada wa hadhara kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Kijiji na fedha zitakazopatikana zitakuwa mali ya Kijiji.

l) Endapo mbao na magogo vitakuwa vimekamatwa Kijiji kitatakiwa kipate ruhusa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Kabla ya kuuza au kutumia vitu hivyo.

m) Endapo mnyama atakuwa amekamatwa, Kijiji kitatakiwa kuwasiliana na Afisa wanyama pori wa Wilaya mara baada ya kumkamata mtu huyo kwa hatua zaidi kama zilivyo katika sheria ya Wanyama pori.

Sheria ndogo hizi zimepitishwa kwenye Mkutano Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa lililokaa tarehe …….. na kusainiwa na

.....

Lipi Y. Benju

Afisa Mtendaji wa Kijiji

Kijiji cha Mchakama

Tarehe.....

.....

Musa A Musa

Mwenyekiti wa Kijiji

Kijiji cha Mchakama

Tarehe.....

.....

Maimuna Mtanda

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa

Tarehe.....

.....

Ally Mtopa

Mwenyekiti

Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa

Tarehe.....

SHERIA NDOGO HIZI ZITAANZA KUTUMIKA RASMI TAREHE 07/11/2014